**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**

**SHULE YA SEKONDARI NYICHOKA**

S.L.P. 176

MUGUMU-SERENGETI

**TAREHE.......................................**

**KumbNa /NYICH/SS/APL/2020/1**

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………..

SHULE YA MSINGI ATOKAYO……………………………………………..

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI NYICHOKA2021**

Nafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza shule ya sekondari NYICHOKA

Nafasi hii ni nyeti umeipata kutokana na ushindi wako wa kumaliza elimu ya msingi (PSLE) hivyo huna budi kuthibitisha hilo kwa kusoma zaidi ili ufaulu mitihani ya sekondari na hatimaye kuendelea na elimu ya juu.

Shule hii iko mkoa wa Mara, Wilaya ya Serengeti katika kata ya kyambahi .shule inapatikana Barabara iendayo BUNDA kutoka katika mji wa mugumu karibu na senta ya Nyichoka .Muhula wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021** ambayo ni siku ya kufungua shule na unatakiwa kufika tarehe hiyo na kuripoti ofisi ya Makamu mkuu wa shule (Second master/ Mistress) ili usajiliwe.

Mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2020 na baada ya hapo hautapokelewa na hivyo utakuwa umepoteza nafasi yako.

Pamoja na fomu hii nimeambatanisha fomu na vielelezo muhimu vinavyotakiwa shuleni kama ifuatavyo;

1. Fomu ya mahitaji ya kujiunga na shule **(soma uyaelewe na kuyatekeleza kabla ya kuja shuleni)**
2. Fomu ya sheria na kanuni za shule (Soma uzielewe, ukubaliane nazo na kuzitii kisha ubaki na nakala hiyo ikuoongoze siku zote)
3. Fomu ya utambulisho, ukubali na ahadi ya mzazi/mlezi (Ijazwe na kusainiwa na wahusika kisha ilete shuleni.
4. Nakala ya cheti cha kuzaliwa na hati ya kiapo mahakamani (Affidavit form) Mzazi aitafute na ailete shuleni ili kuthibitisha kuzaliwa na uraia wa mwanafunzi.
5. Fomu ya kuthibitisha afya ya mwanafunzi (medical examination form) mwanafunzi athibitishe hali ya afya kwa daktari na fomu hii irudishwe shuleni ikiwa imejazwa, kusainiwa na kugongwa muhuri wa Mganga Mkuu wa Wilaya. (DMO)
6. Mtengenezee mwanao **Kiti** na **Meza** kwa sababu shule ina uhaba wa samani.

**.....MKUU WA SHULE........**
NYICHOKA SEKONDARI
**MODESTER C. WILLIAM**

**FOMU YA MAHITAJI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYICHOKA.**

1. **SARE ZA SHULE**
   - A. Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi kwa wavulana na wasichana (yawe na mfuko mmoja tu upande wa kushoto)
   - B. (i) Suruali mbili (2) kwa wavulana za light blue (blue Bahari) zenye marinda mawili 2 tu na mkanda wa ngozi mweusi na tai ya light blue.

     (ii) Sketi mbili kwa wasichana zenye marinda boksi (2 mbili mbele na nyuma)na malinda madogomadogo pembeni ziwe ndefu mpaka kwenye vifundo vya miguu pamoja na tai ya light blue.
   - C. Viatu vyeusi jozi mbili visivyo na visigino wala umbo la buti ( kiaskari) na sharti viwe vya kamba.
   - D. Soksi jozi mbili au Zaidi ndefu nyeupe kwa wasichana na ndefu nyeusi jozi mbili au zaid kwa wavulana
   - E. Sweta la mikono mirefu **rangi** nyeusi lenye umbo la "V"kifuani
   - F. Nguo za michezo ni Track Suit rangi ya (Dark blue) na raba za michezo (kwa wavulana na wasichana)

**ANGALIZO**

- Kitambaa cha sketi na suruali (rangi na material yake) kimeambatishwa usinunue tofauti na rangi hiyo.
- Wasichana wa kiislamu wana haki ya kushona mavazi yanayoendana na Imani yao ikiwemo hijabu isipokuwa sharti yaendane na vitambaa vya sare za shule pasipo urembo wowote.

**MAHITAJI YA USAJILI, TAALUMA, CHAKULA NA VIFAA VYA USAFI**

- **TAALUMA**

1. Rimu moja ya karatasi ya A4 aina ya Double A ( kwa ajili ya matumizi ya mitihani , majaribio na uchapaji nyaraka kwa wazazi au walezi (ALETE SHULENI SIKU ANAPORIPOTI)
2. Madaftari makubwa (counter book kumi 10), kalamu za kutosha, penseli, rula, bofa au mathematical set na kifutio.
3. Vitabu binafsi vya kujisomea shuleni japo shule inavyo
4. Kamusi ya kingereza (Dictionary)

- **VIFAA VYA USAFI**

(I) WASICHANA
- (a) Mifagio mirefu ya ndani ya kununua dukani (hard bloom)
- (b) Ndoo ya lita kumi 20 kwa ajili ya kuchotea maji
- (c) Reki na miche mitano ya miti ya kimvuli.

(II) WAVULANA
- (a) Fyekeo kwanja
- (b) Jembe na mpini wake
- (c) Miche mitano(5) ya miti.

..................................

MKUU WA SHULE
NYICHOKA SEKONDARI

MODESTER C. WILLIAM

# KIAMBATANISHO "B"

## FOMU YA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule ya sekondari Nyichoka inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Mama ya Elimu NO.25ya mwaka 1978 pamoja na marekebisho yake kwa miaka ya hivi karibuni .Aidha shule iko chini ya Wizara ya Elimu ya Mafunzo (WEMU) na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa (TAMISEMI )ikimilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ,Zifuatazo ni baadhi ya sheria na kanuni ambazo sharti kila mwanafunzi azitii na kuzifuata kwa muda wote wa uwanafunzi wake .

### I. MAMBO AMBAYO NI LAZIMA YATEKELEZWE /KUTII

1. Kuheshimu watu wote wanaomzidi umri wakiemo viongozi ,wazazi ,wanafunzi /walimu
2. kusimamia na kusalimia mtu yeyote anayemzidi umri anapopita
3. .Kuwahi shuleni na katika shughuli zozote atakazopewa ikiwa ni pamoja na kuwahi kutoka mapumziko ya likizo
4. Kuwa na mahudhurio mzuri (ya kila siku )kwa shughuli zote za ndani na nje ya darasa siku zote za shule .
5. Kufahamu mipaka ya shule na ni marufuku kutoka nje ya mipaka ya hiyo bila ruhusa kwa siku zote ajapo shule
6. Kushiriki kikamilifu shughuri za nje ya darasa kama vile michezo ,usafi wa mazingira ,kilimo \miradi n.k.
7. Kutunza usafi wa mwili kwa kutofuga kucha ,ndevu,kutopaka rangi au chapa ya mwili ,kutofua nguo (uniform) na kuweka mzingira ya shule yawe safi daima.
8. Kuvaa sare za shule wakati wote awapo /ajapo na atokapo shuleni .
9. Kuzingatia ratiba ya shule na kufanya kazi zote za darasa ikiwepo mitihani ,majaribio na mazoezi yatolewayo.
10. Kutoleta shuleni /kutumia simu ya mikononi na /aukujihusisha na vikundi viovu (makundi ya shinikizo rika).
11. Kutumia lugha ya kiingereza /au Kiswahili wakati wote wa kuwasiliana shuleni.

### II. MAMBO AMBAYO YANAWEZA KUSABABISHA AFUKUZWE SHULE MARA MOJA

1. Wizi wa aina zote
2. Uasherati ,ushoga na ubakaji
3. Uvutaji ,ulevi au matumizi ya madawa ya kulevya k.v bangi, mirungi ,kubeli,sigara,cocaine n.k
4. Kupigana au kupiga au kumnyanyasa mwenzake
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule au umma
6. Kudharau bendera au wimbo wa Taifa na viongozi wote .
7. Kuoa au kuolewa ,kupata/kuharibu mimba au kumpa mimba yeyote.
8. Kugoma ,kuchochea au kushiriki migomo yoyote ndani au nje ya shule
9. Kukataa adhadu aliyopewa kwa makusudi
10. Kukutwa baa,vilabu vya pombe ,kumbi za starehe (Disco )na kuingia ofisi za walimu,bwalo la chakula .jiko .stoo n.k bila ruhusa /sababu maalum,ya kuepo hapo.

# KIAMBATANISHO C

## FOMU YA UTAMBULISHO ,UKUBALI NA AHADI YA MZAZI

## IJAZWE KIKAMILIFU NA KURUDISHWA SHULENI

### I. MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI (UTAMBULISHO)

i. Jina kamili ......................................................................................

ii. Tarehe ya kuzaliwa ......................................................................................

iii. Kabila ......................................................................................................

iv. Shule ya msingi aliyotoka ......................................................................

v. Mahali/mtaa/kijiji anapotoka kuja shuleni
.................................................................

vi. Mahali /kijiji wazai wake wanapoishi
......................................................kata ...............................Wilaya
.......................................................................................................

vii. Jina kamili la Baba /Mlezii
.......................................................................................................

viii. Jina kamili Mama /
Mlezi.......................................................................................................

ix. Kazi ya
Baba/mlezi.......................................................................................................

### II. AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi.......................................................................................nimesoma na kuelewa sheria na kanuni za shule ya sekondari Nyichoka na kukubaliana nazo .Naahidi kufuata taratibu zote za shule na kutii sheria ,kanuni na maelezo yote yatakayotolewa kwangu na uongozi wa shule .Sitashiriki vitendo vyote viovu wala kushiriki migomo na kwa kadri ya uelewa wangu naahidi kushirikiana na shule kufichua wanafunz i wenzangu wanaokusudia kufanya uovu shuleni ili wachukuliwe hatua .

SAINI YA MWANAFUNZI ......................................................................................

### III. AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi ......................................................................................................Ambaye ni ...............................................................(taja uhusiano wako )wa mwanafunzi ...............................................................nimeyasoma maelezo ya kujiunga na shule ya sekondari Nyichoka pamoja na kanuni na sheria zake .Naahidi kwamba nitajitahidi kusaidiana na uongozi wa shule kumhimiza mwanangu kutii sheria za shule na kumpa malezi bora .

JINA LA MZAZI /MLEZI ......................................................................................

SAINI YA MZAZI /MLEZI ......................................................................................

### IV. UTHIBITISHO WA MKUU WA SHULE

Mwanafunzi na Mzazi /Mlezi wake wametoa ahadi yao mbele yangu na hiyo Kukubaliwa kusoma kwa masharti tajwa

**SAINI** [signature]

................................................................................**MHURI**...MKUU WA SHULE NYICHOKA SEKONDARI............

**KIAMBATANISHO D**

**MEDICAL EXAMINATION FORM (UTHIBITISHO WA AFYA)**

(IJAZWE NA DAKTARI NA MWANAFUNZI AIRUDISHE SHULENI)

Student's Full Name ______________________________

Age ______________ Height (cm) ____________ Weight (kg) ______________

(To the doctor/medical officer concerned: Please, examine the above student who has been selected to join secondary education to see his/her Physical fitness to pursue with the secondary education and give us your comments for further considerations)

1. Blood count ______________________________
2. Stool examination ______________________________
3. Urinalysis ______________________________
4. Sexual Transmitted Infections/HIV ______________________________
5. TB and Leprosy Test ______________________________
6. Eye test ______________________________
7. Ear test ______________________________
8. Chest test ______________________________
9. Abdomen Test ______________________________
10. Plano test (Girls) ______________________________
11. Spleen test ______________________________
12. Additional information e.g. Physical defects or impairments infection, chronic or family disease like circle cell, inability to eat certain food etc.

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

I certify that, I have examined the above named student and found her/him to be fit to pursue secondary education.

SIGNATURE ______________________________

DOCTOR'S NAME ______________________________

STATION ______________________________